

Usalama ya Intaneti



Unyanyasaji ya ku mutandao

Unyanyasaji ya ku mutandao inaweza jitokeza fasi yote yote ku mutandao.

Unyanyasaji ya ku mutandao ni wakati mutu anatumia teknolojia kwa makusudi na mara kwa mara ili kumushusha, kumuumiza ao kumusababisha mutu mwengine maumivu kupitia kompyuta, simu za mkononi na vifaa ingine ya kielektroniki.



Gisi ya kukabiliana na unyanyasaji ya ku mutandao:



Ambiya mutu muzima

Vijana wanapashwa kila mara kuelezea mutu muzima mwenye wanaaminiya kusudi watafute mbinu za kukabiliana na hali.



Kusanya ushahidi

Weka ujumbe ao ukamate picha kama ushahidi, lakini USIJIBIYE ku azo wala kuzivuta.




Tafuta msaada ya zaidi

Wajulishe viongozi wa masomo ao polisi wakati inahitajika.









Linda Habari Zako za Kibinafsi

- Usipatiye mutu yeyote habari zako za kibinafsi, sawa vile namba yako ya Usajili ya Mugeni, namba yako ya Hifazi ya Jamii, maneno ya siri ao picha zako.
- Mbele ya kubofya ao kufungula faili yenye iliambatanishwa, hakikisha barua pepe ao ujumbe imetoka kwa mutu ao fasi ya kuaminika.
- Kuwa mwangalifu na njia za kuiba habari zako; mutu wa udanganyifu anaweza kujifanya kuwa wa kuaminika, sawa vile IRS, benki, matangazo ya kupana kazi ya bongo, na kazalika.



Kuwa Mwangalifu ku Mitandao ya Kijamii



Fuata akaunti zenye zinaboresha maisha yako na zenye zinahusiana na mambo yenye unapendaka na yenye inakuvutiaka.

- Afya ya Mwili/Afya ya Akili (kwa mufano, Headspace)
- Kujenga kujiamini na kujisamini (kwa mufano, WeTheUrban)
- Kukamata picha (kwa mufano, Eartpix)
- Muchezo ya Kabumbu (kwa mufano, Bestofffootball)
- Kucheza dansi (kwa mufano, Renatobailarinos)



Kwa ajili ya Wazazi na Walezi:

Zungumuza na kijana wako kuhusu Usalama ya Intaneti.

- Kuwa wazi, sema ukweli, na usifiche hisia zako wakati unazungumuza kuhusu usalama ya intaneti.
- Zungumuza kwa utulivu na usijibiye mubaya ku maoni ya kijana.
- Muelimishe kijana pahali ya kumutia boga.

